**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA ESTHER N. MATIKO KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS MAHUSIANO NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016

Ofisi ya Bunge,
S. L. P 941,
**DODOMA**

Mei, 2015.

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI MHESHIMIWA ESTHER N. MATIKO KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA 2014/2015 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS MAHUSIANO NA URATIBU KWA MWAKA WA FEDHA 2015/2016**

## UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, toleo la 2013, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya 2014/2015 na makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais Mahusiano na Uratibu kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru familia yangu, wana Mara na watanzania wote kwa ujumla kwa kuwa nami bega kwa bega. Kipekee zaidi napenda kuwashukuru wana Tarime kwa kushirikiana nami na kwa imani kubwa waliyo nayo kwangu. Nawaahidikutowaangusha Oktoba 2015, lazima kieleweke.

## Maoni ya Jumla ya Mahusiano na Uratibu

**Mheshimiwa Spika**, jamii yoyote inayojengwa katika misingi ya kuheshimu uhuru wa watu wake katika imani yao juu ya uwepo wa Mungu na kukubai kufuata taratibu za nchi katika kuchagua imani yoyote isiyovunja Sheria, ni jamii yenye uwezo mkubwa wa

kushinda majaribu yoyote na misukosuko dhidi ya watu wake. Ikumbukwe kuwa, mwaka 2005 Taifa likiwa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, wabunge na madiwani, viongozi wa dini walitamka kuwa Mheshimiwa Rais ni Chaguo la Mungu. Hakuna kiongozi yeyote wa wakati ule, na si Rais Kikwete mwenyewe wala Chama chake ambao waliwataka Vongozi wa dini kuacha kujihusisha na siasa.

**Mheshimiwa Spika,** ikiwa imepita takribani miaka 10 toka kauli ile ya kumuidhinisha Rais Kikwete katika masuala ya dini ; ambaye pia mara kwa mara ameendelea kuwatumia viongozi wa dini kuhalalisha masuala yenye ukakasi kwenye Jamii, hivi karibuni Rais Kikwete ambaye alitoa kauli akiwataka viongozi wa dini kutojihusisha na siasa. Ni dhahiri kuwa kauli ya Maaskofu kuwahamasisha waumini wake kuikataa Katiba pendekezwa imeiumiza Serikali na ndio maana Serikali imeenda mbali zaidi na kutoa hata tishio kupitia Waziri wa Mambo ya Ndani Mheshimiwa Mathias Chikawe kuwa watazifuta taasisi za dini nchini. Kauli hizi ni kauli za hatari ambazo si tu zinalenga kuwafunga viongozi wa dini midomo bali pia zinahatarisha usalama wa taasisi za kidini na waumini wake kuelekea uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015.

**Mheshimiwa Spika**, ni Serikali hii ya CCM iliyoshindwa kudhibiti vurugu za kidini ikiwemo kuchomwa kwa makanisa na

kuuawawa kwa viongozi wa dini Zanzibar, kukojolewa kwa Qoran Tukufu kule Mbagala ambapo kulisababisha vurugu, kulipuka kwa mabomu Arusha katika makanisa pamoja na mgogoro wa uchinjaji nchini. Ni mambo ambayo kwa mara ya kwanza tumeyashuhudia katika Serikali ya awamu ya nne ambayo kwa muda mrefu imekua ikitoa tuhuma za kidini na kuchochea ugomvi wa kidini kwa kuvipaka matope vyama vya Upinzani kuwa ni vya udini ilhali viongozi wake kwa kauli zao wamekua wakipasua taifa kwa udini. Ni ishara kuwa jukumu la ulinzi na usalama kwa makundi yote nchini hasa makundi ya kidini upo mashakani. Ni vema Serikali sasa ikapumzika maana imechoka kusimamia masuala muhimu kwa ajili ya Utengamano wa taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu sasa Serikali ya Chama cha Mapinduzi imekuwa ikizitumia taasisi za dini kama njia ya propaganda na kuwahadaa watanzania. Walifanya hivyo kwenye uchaguzi Mkuu wa 2005 ikiwemo kuwaahidi Waisalmu kupitisha mahakama ya Kadhi, walifanya hivyo kwenye uchaguzi wa mwaka 2010, walifanya hivyo kwenye Bunge Maalumu la Katiba, Walifanya hivyo kwenye Muswada wa Mabadiliko wa Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2015 ambapo tulishuhudia kwenye baadhi ya vyombo vya habari jinsi

ambavyo wabunge wa Bunge lako wakigawanyika wakiwemo wabunge wa CCM wao kwa wao.

**Mheshimiwa Spika,** ni bahati nzuri sasa kuona kuwa viongozi wa dini wameamua kutokuwa sehemu ya kuwahadaa watanzania. Viongozi walio wengi wameamua kusimamia maslahi ya taifa kwa manufaa ya watu wote nchini. Viongozi wa dini wengi wamekataa kutumika na Serikali ya CCM katika kuwagawa Watanzania kupitia udini. Ndio maana baadhi ya Viongozi wa dini sasa wameamua na kusema, sasa yatosha. Viongozi wa dini sasa wameamua kusimamia maslahi mapana ya Watanzania ikiwemo kuwapa elimu ya kuikataa Katiba Pendekezwa iliyochakachuliwa na Serikali ya CCM.

Aidha, ni aibu kwa Serikali ya Rais Kikwete kuingilia faragha ya waislamu waliokua katika Hijja, Makka kwa kutumia mamilioni ya Watanzania na kudai kuwafata mahujaji hao kwa ajili ya kupigia kura kwa kile kinachoitwa Katiba Pendekezwa. Pengine Serikali hii inayotaka kutenganisha masuala ya dini na siasa leo pia imesahau kuwa walioshiriki katika Mchakato huu wa Katiba waliapa kwa kutumia dini zao. Ni katika mchakato huu ambao Matokeo yalichakachuliwa ikiwemo suala la Makamu Mwenyekiti wa NCCR- Mageuzi Mheshimiwa Haji Khamis Ambari alihesabiwa kupiga kura huku akiwa hajapiga kura.

**Mheshimiwa Spika,** kambi ya Upinzani Bungeni inahitahadharisha Serikali kutozigusa taasisi za dini hasa ambazo zimeendelea kutoa elimu kwa watanzania bila kuvunja taratibu za nchi hii. Aidha, tunawahasa viongozi wa dini zote na waumini wao kutokubali mpango huu ovu wa Serikali ya CCM unaopanga kupoka haki yao ya kikatiba na uendeshaji bora wa taasisi zao.

**Mgogoro wa Madereva Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa Serikali inajukumu la kuratibu mahusiano ya makundi mbalimbali ya kijamii, kumekuwepo mgogoro mkubwa unaosababishwa na kukosekana kwa imani baina ya Serikali na Madereva kuhusu namna ya kusimamia maslahi yao. Kimsingi ni kweli kuwa Serikali haiajiri madereva kwa magari ya watu binafsi hasa wale wa magari ya abiria na magari ya mizigo. Lakini sote ni mashahidi jinsi ambavyo kulikuwa na usimamizi mbovu wa Serikali kuhusu madai ya madereva na adha ambayo wananchi waliipata mara mbili mfululizo kwa migomo ambapo awali madereva waligoma baada ya kutakiwa kusoma kila wanapoomba leseni upya katia Chuo cha Usafirishaji (NIT). Aidha, mgomo mwengine ulisababishwa na madai ya madereva juu ya mikataba na ujira wa kazi yao dhidi ya waajiri ambao ni wamiliki wa magari.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kauli mbalimbali za viongozi na mawaziri ambao walizitoa kwa madereva hao, ni dhahiri kuwa Serikali haijaweka mkakati wa kudumu kuhakikisha maslahi ya pande zote mbili za mgogoro yanalindwa bali mgogoro huo unatumiwa na Seriali kama chambo cha kujipatia kura kwenye Uchaguzi Mkuu ujao. Na ikumbukwe kuwa, ujanja unaofanywa na Serikali ndio uliopelekea kutaka kupigwa kwa Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni ambaye ilibidi afichwe na kulindwa na askari polisi kwa usalama wake Kituo cha Mabasi yaendayo Mikoani cha Ubungo .

Kambi ya Upinzani Bungeni inapenda kuchukua fursa hii kuwataka madereva wote kuwa wavumilivu kwa kuwa, madhara ya migomo si tu inayumbisha uchumi bali pia ina athari kwa watanzania mafukara ambao wengi ndio tunaotumia usafiri wa umma kwa ajili ya shughuli zetu za kila siku. Aidha, natumia rai ile ile aliyotoa Kiongozi wa Upinzani Bungeni Mheshimiwa Freeman Mbowe pamoja na Mwenyekiti Mwenza wa UKAWA kutoka CUF Prof. Ibrahim Lipumba ambao waliwafuata mlipokua na kuwasikiliza, kuwa hakuna marefu yasiyo na ncha. Kipindi hichi ni vyema kwa madereva wote na abiria wanaotumia usafiri wa umma kutafakari ni jinsi gani wameendelea kutumika na Serikali ya CCM. Ni dhahiri kuwa nguvu kubwa ya kufanya mabadiliko nchini itatokea iwapo

watanzania tutashikamana, tutajiandikisha kwa wingi katika daftari la kudumu la wapiga kura na kujitokeza kwa wingi katika zoezi zima la Uchaguzi Mkuu Oktoba na kuchagua UKAWA popote pale mlipo.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali itakayoundwa na Umoja wa Vyama vya Upinzani (UKAWA) inaendelea kuamini kuwa kila mtanzania ana haki ya kutoa maoni yake kwa njia ambayo anaona itapata usikivu wa watawala. Nasi kama UKAWA, tumeandaa Sera na miongozo itakayohakikisha uwepo na upatikanaji wa mazingira mazuri ambayo yataleta haki kwa kila mmoja wa madereva ambao hufanya kazi katika mazingira magumu. Ni dhahiri kuwa Serikali imelilea tatizo hili kwa muda mrefu na pia imeendelea kutoa ahadi za uwongo kwa madereva kupitia kwa Waziri wa Kazi jambo ambalo lilisababisha mgomo kwa mara ya pili na kuleta adha kwa wananchi katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, Kambi ya Upinzani Bungeni inawasihi wamiliki wa mabasi na vyombo vya usafirishaji ikiwemo malori kutafuta suluhu ya kumaliza mgogoro huu ambao una athari za kiuchumi si tu kwa dola bali hata kwao binafsi kama wafanyabiashara. Ni tumaini letu kuwa wamiliki wa vyombo vya usafiri watafanyia kazi mazingira ya utumishi wa madereva ili kujenga uaminifu na mauhusiano bora baina yao na waajiriwa wao.

## Mgomo wa Wafanyabiashara

**Mheshimiwa Spika,** katika utawala wa awamu ya nne ni dhahiri kuwa Serikali ilidhamiria kutowashirikisha wananchi kikamilifu katika maamuzi mbalimbali yanayoathiri shughuli zao za kila siku na hivyo kukosa imani kwa wananchi. Ulipaji wa kodi hauepukiki kwa Taifa lolote lile duniani. Kodi za wananchi zimeendelea kuwa chanzo kikubwa cha mapato ili zitumike katika utoaji huduma za wananchi. Kwa nchi nyingi za kiafrika, ulipaji wa kodi umekua hauendani na utoaji na upatikanaji wa huduma muhimu zikiwemo maji, elimu, huduma za afya, makazi, miundombinu na kadhalika, kwa kuwa Serikali zimeendelea kuwa na matumizi makubwa na hivyo kuzua malalamiko hasa kutoka kwa walipa kodi wakiwemo wafanyabiashara.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi makubwa ya Serikali ya CCM, ubadhirifu pamoja ufisadi mkubwa, vimejenga mazingira ambayo walipa kodi hawana imani na mifumo ya Serikali ya ulipaji wa kodi. Wafanyabiashara wametafsiri mifumo ya ulipaji wa kodi kama njia mojawapo ya unyonyaji unaofanywa na Serikali ya CCM. Kudhihirisha hili, Katibu Mkuu wa CCM abdulrahman Kinana alitaja utitiri wa kodi za Tanzania kama kikwazo cha wafanyabiashara kufanikiwa. Ndugu Kinana alitoa kauli hiyo mwezi April 2015 kwenye mkutano wa hadhara katika Viwanja vya Pasua mjini Moshi.

**Mheshimiwa Spika,** ni katika mkutano huo ambao Katibu Mkuu wa CCM ambaye Mwenyekiti wake ndiye Raisi alisema kuwa wafanyabiashara wanaumizwa zaidi na kodi hizo lakini hawana mtu wa kuwasemea zaidi ya kuendelea kunyonywa. Vilevile, kama kawaida yake Katibu Mkuu huyo aliwatupia lawama wabunge wa CCM kuwa wingi wao bungeni hausaidii kitu kwa sababu wameshindwa kuondoa sheria zinazomkandamiza mwananchi.

> "***Kila kona ni kodi na kila kukicha ni kodi, Sumatra anadai kodi, Fire wanadai kodi, taasisi zingine zinadai kodi, yaani ni kero tupu***"

**Mheshimiwa Spika,** kauli ya Katibu Mkuu wa CCM Kinana inathibitisha madai ya muda mrefu ya wafanyabiashara nchini juu ya kunyonywa kwao na mifumo holela ya kodi. Ni katika kadhia hii ambayo imesababisha mara kwa mara wafanyabiashara kuendelea kugomea mashine za kieletroniki za ulipaji wa kodi kitaalamu zinajulikana kama EFDs. Mashine hizi zinazotolewa na TRA zinatolewa kwa gharama kubwa na pia kiwango cha asilimia 18 kimeonekana kuwa kikubwa kwa wafanyabiashara. Ni katika kadhia hii hii ndiyo iliyopelekea kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa Mwenyekiti wa Jumuia ya Wafanyabiashara Tanzania, Johnson Minja (34) kwa

madai ya uchochezi wa kuwataka wafanyabiashara kugomea matumizi ya EFDs Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** mpaka leo kumeendelea kuwepo kwa migomo baridi inayofanywa na wafanyabiashara maeneo mbalimbali nchini, kama njia ya kushinikiza kufutiwa kesi kwa kiongozi wao huyo. Vile vile, migomo hii imeendelea kuleta athari kwa walaji kwa kuwa wafanyabiashara wamekuwa wakifunga maduka mara kwa mara. Lakini Serikali kwa nyakati tofauti hata kwa kauli ya Waziri Mkuu Mizengo Pinda imeonesha wazi kutotaka suluhu na wafanyabiashara ikiwemo kumfanyia hila Ndugu Minja na kumuweka rumande wakati ambao Serikali imedai inafanya maridhiano na wawakilishi wa wafanyabiashara nchini.

Kambi ya Upinzani Bungeni, inasimama pamoja na wafanyabiashara wote nchini na kuwataka kusimama imara katika kupigania maslahi yao. Aidha, tunaendelea kutumia wataalamu wetu mbalimbali ambao wanatoa elimu juu ya umuhimu wa ulipaji kodi nchini. Ni kwa misingi bora ya uwajibikaji inayotupa imani kuwa watanzania watatupa dhamana ya kuwaongoza ili kuhakikisha kuwa kuna uwazi na uwajibikaji katika matumizi na mapato ya Serikali hasa kodi za wananchi wa Tanzania.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inawataka wananchi kuchagua Serikali itakayotokana na Umoja wa Vyama vya Upinzani "UKAWA" ili iweze kutoa elimu sahihi na msaada kwa wafanyabiashara na walaji , itakayowawezesha kushiriki katika utoaji wa huduma bora kwa kulipa kodi kwa mfumo utakaodhibitiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Tunawaahidi watanzania kuwa, kodi zao hazitopotea bure na tutawajibikiwa kwa kuandaa mifumo ya wazi itakayochambua mapato na matumizi ya Serikali ya UKAWA.

**Wanafunzi wa Elimu ya Juu Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** kwa muda mrefu Serikali ya CCM imeshindwa kuisimamia ipasavyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Nchini (HESLB). Hii inatokana na Serikali kuchelewesha kupeleka fedha wa ajili ya wanafunzi na hivyo kufanya Bodi ishindwe kufanya kazi kwa ufanisi. Matokeo ya ucheleweshaji wa mikopo kwa wanafunzi imezua migogoro mingi ikiwemo migomo ya wanafunzi, kusimamishwa kwa wanafunzi ama wanafunzi kuzuiwa kufanya mitihani ama kukatishwa masomo kwa kushindwa kulipa ada mbalimbali za vyuo. Aidha, kumekuwa na misigano ya muda mrefu baina ya Wanafunzi na utawala wa

vyuo mbalimbali na misigano hii huleta athari kubwa kutokana na Serikali kushindwa kuisimamia ipasavyo. Kwa mfano migogoro na migomo ya vyuo vya UDOM, UDSM, MUHAS iliyopata kutokea katika utawala wa Rais Kikwete ni kielezo kuwa Serikali bado imeendelea kuchukua hatua dhidi ya matokeo badala ya kushughulikia vyanzo vya matatizo hivyo kuacha madai ya msingi ya wanafunzi wa vyuo hivyo yakipuuzwa. Ni wanavyuo wengi ambao wamesimamishwa vyuo, kuna waliosababishiwa ulemavu, wengine wakishindwa kurudishwa vyuoni na wengine wakiwa hawajui hatma ya masomo yao kutokana na matatizo ama madai yao kutopatiwa ufumbuzi wa kudumu.

**Mheshimiwa Spika,** ikumbukwe kuwa mwaka 2007 Rais Jakaya Kikwete aliahidi kuyapatia ufumbuzi matatizo ya wanafunzi wa elimu juu nchini ili kupunguza migomo na migogoro. Katika Mkutano wake na wanafunzi wa vyuo vikuu wa CCM mwezi Februari 2007 alikwenda mbali zaidi kwa kuwaeleza kwamba hakuna mtoto wa maskini atayeshindwa kuendelea na masomo kutokana na masharti ya mikopo. Ikiwa ni miaka 8 imepita toka ahadi hizo zitolewe migomo katika vyuo vikuu imeendelea na pia wapo watoto wa walalahoi ambao wamefaulu kidato cha sita lakini wemeshindwa kuendelea na masomo kutokana na kukosa mikopo na upendeleo wa wazi katika upangaji wa

viwango vya madaraja ya mikopo nchini usiozingatia vigezo vilivyowekwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inachukua nafasi hii kuwaeleza watanzania wote na watoto wa kitanzania kuwa, Umoja wa Vyama vya Upinzani "UKAWA" bado inaamini kuwa ikiwa Mwalimu Nyerere aliweza kuwasomesha watoto wa wakulima mpaka elimu ya juu basi nasi tutaweza kutoa elimu bure kwa watanzania wote bila kujali rangi, dini, kabila wala madaraja yao katika jamii. Ni rai yetu kubwa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kukataa kutumika pamoja na kuhadaika na ahadi kemkem za CCM bali watumie fursa hiyo kujiandikisha kwa wingi katika daftari la kudumu la wapiga kura mwaka huu popote walipo na kupiga kura Oktoba 2015. Tuwakumbushe pia vijana wote waliokosa fursa za masomo kutokata tamaa kwa kuwa nchini Nigeria, vijana ndio waliofanikisha kuundoa utawala wa Rais Goodluck Jonathan na kufanikisha ushindi wa Rais Buhari. Hivyo hii ni fursa pekee ya kuwaepusha na maumivu makali ya miaka mitano mingine iwapo watafanya makosa kuirudisha CCM madarakani Oktoba 2015.

## Migogoro Kati ya Wakulima na Wafugaji

**Mheshimiwa Spika**, katika miaka 10 ya mateso ya awamu ya nne kumeibuka migogoro kati ya wakulima na wafugaji hasa katika sehemu za Morogoro, Rufiji, Kongwa, Babati, Arusha n.k.

Kwa muda mrefu tumekuwa tukipendekeza mara kadhaa njia za kuchukua kuondokana na jambo hili kwa serikali kuchukua hatua mahsusi za kupima ardhi nchi nzima na kuyatambua maeneo kwa ajili ya matumizi kwa makundi haya lakini bado tumeendelea kushuhudia migogoro hiyo kuendelea kugharimu maisha ya watanzania masikini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapenda kusema kuwa, sasa imetosha na ni wazi kuwa Serikali imeshindwa kutatua tatizo hilo.

**Serikali kutishia NGO Zinazotekeleza Majukumu Yake**

**Mheshimiwa Spika,** mojawapo ya dalili za Serikali inayoshindwa ni pamoja na kuogopa Kivuli chake chenyewe. Serikali hii ambayo imetumia fedha nyingi na nguvu nyingi katika kuhalalisha maovu yake imejikuta ikishindwa na nguvu ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs) ambazo kwa kiasi kikubwa zimeweza kuonesha madhaifu ya Serikali kwa kutoa elimu kwa watanzania wote kinyume na matarajio ya Serikali. Ni hivi karibuni mkoani Geita Januari mwaka huu Mashirika zaidi ya 1000 yasiyo ya kiserikali nchini Tanzania yalitangaziwa kufutwa kwa usajili wake kunatokana na kutotimiza matakwa ya kisheria katika utendaji wake kazi toka yaliposajiliwa. Ni kwa mujibu wa kikao cha bodi ya uratibu ya mashirikia yasiyo ya kiserikali ambacho kilieleza kuwa kufutwa kwa mashirika hayo kutokana na kushindwa kutoa taarifa za kila mwaka kama inavyosisitizwa

na Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na 24, 2002. Mashirika hayo pia yanadaiwa kukosa sifa ya kuendelea kufanya kazi kwa mujibu wa sheria nchini Tanzania.

**Mheshimiwa Spika**, ikiwa inaelekea ukingoni, Serikali ya CCM inakumbuka shuka kumekucha huku kwa kipindi cha miaka 10 ya utawala wake kikishindwa kukagua utendaji wa mashirika hayo. Ni matumaini yetu kuwa, Serikali hii haitoisahau Taasisi ya Wanawake na Maendeleo (WAMA) inayoongozwa na Mke wa Rais, Mama Salma Kikwete, ambayo nayo ilikiuka masharti na kanuni za uendeshwaji kwa kuwa Waziri (Mhe. Sophia Simba) mwenye dhamana ya kuzisimamia taasisi zisizokuwa za kiserikali kuwa Mjumbe wa Bodi ya WAMA. Ikiwa Serikali imeamua kusafisha mashirika hayo yasiyo ya Kiserikali isisahau kuifutia WAMA usajili wake kwa kukiuka Sheria za nchi.

**Hali ya Usalama Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** hali ya Usalama nchini sio nzuri na hivyo ni dhima ya Serikali mpya ijayo itakayoundwa na upinzani kuboresha kitengo cha usalama wa Taifa kuliko hali ilivyo sasa. Hii ni kutokana na ufisadi mwingi kuendelea kujitokeza nchini na kushindwa kuzuiliwa na kitengo hiki kwa maslahi ya taifa zima. AIDHA, mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ulemavu wa ngozi yameendelea kulitikisa taifa. Ni jambo la kushangaza kuwa Usalama wa Taifa unashindwa kutoa taarifa za kiinteljensia

kuhusu ukatili kwa kundi hili la watu wasiozidi 200,000 nchi nzima. Jambo la kusikitisha zaidi, yakiwa yamepita si chini ya masaa 48 tangu Waziri Mkuu Pinda asome hotuba yake ya kukabiliana na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi tarehe 12 Mei 2015, tukio la kusikitisha la kukatwa kwa mkono kwa mwanamama Remi Luchoma (30) limetokea kwenye mkoa wa Katavi, tarehe 14 Mei 2015 anapotoka Waziri Mkuu mwenyewe. Hii ni aibu kubwa kwa utawala wa CCM na Rais Kikwete.

**Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

**Mheshimiwa Spika**, Kitendo cha Chama Cha Mapinduzi kushindwa kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa kiwango kikubwa kuliko matarajio yake na kulazimisha kuapishwa kwa viongozi wake ambao wananachi hawakuwachagua kulipelekea pia kwa baadhi ya viongozi wa Serikali za Mitaa na wakazi wake kuchukua jukumu la kuwaapisha viongozi wao wenyewe. Jambo hili lilisababisha vurugu na taharuki kubwa miongoni mwa wananchi ambao walikuwa wanapinga kuchakachuliwa matokeo na Serikali ya CCM. Jambo hilo linatoa picha juu ya kitakachotokea katika uchaguzi wa mwaka huu ambapo kwa uhalisia ni kuwa Chama cha Mapinduzi hakiko tayari kuachia ngazi hata pale ambapo wananchi wamekikataa. Kwa vyovyote vile Jambo hili litahatarisha amani na utulivu katika nchi. Tunapenda kuwakumbusha CCM na

vibaraka wake kuwa, haki haiporwi bali hucheleshwa na watanzania sasa wameamka.

**Mahusiano ya Vyama vya Siasa**

**Mheshimiwa Spika,** katika awamu hii ya nne ya miaka kumi ya uchungu na maumivu makali tumeshuhudia kuwepo kwa mahusiano yasiyoridhisha kati ya vyama vya siasa hasa uhasama na kushambuliana kwa silaha na vitisho wakati wa chaguzi kuu na chaguzi ndogo. Tumeshuhudia kuchomwa kwa ofisi za Chama cha Wananchi CUF huko Zanzibar, kuumizwa kwa viongozi wa vyama vya upinzani katika maeneo mbalimbali nchini na hata baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa vya upinzani kubambikiwa kesi zinazotokana na uchaguzi. Jambo la kushangaza na kustaajabisha, ni kuwa hakuna mwanaCCM yeyote ambaye amekumbwa na kesi za kudhuru zinazohusiana na chaguzi ambazo zimefunguliwa na Jamhuri bali ni wanasiasa wengi wa upinzani ambao mpaka sasa wana kesi zinazotokana na chaguzi za mwaka 2005 na 2010. Kwa vyovyote vile kukithiri kwa vitendo hivi ndiko kunakolazimu vyama vya siasa kuwa na utaratibu wa kulinda mali na viongozi wao kwa gharama zao wenyewe. Na ni kwa kushindwa huko kwa Serikali kulinda vyama kunapotupa sababu ya kujilinda wenyewe kwa mifumo yetu kama ambavyo CCM inafanya kwa kuratibu na kuendesha kikosi chake cha Ulinzi cha Kijani (Green Guard) kwa kuwa nao

CCM hawana imani na mfumo wa ulinzi na usalama wa Serikali yake yenyewe.

**Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011-2016)**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ya CCM kwa mbwembwe kubwa katika mwaka wa fedha 2011/2012 iliwasilisha Bungeni Mpango wa Miaka mitano ambao ulizinduliwa na Rais Jakaya Kikwete ambao hata hivyo katika mipango na bajeti za kila mwaka tuliweka bayana namna ambavyo Serikali imekuwa haifuati mpango huo. Jambo hilo linadhihirika sasa ambapo mipango mingi ambayo ilikuwa kwenye mpango ule haijatekelezwa na hata bajeti za Serikali hazifuati vipaumbele kama ambavyo vimeainishwa kwenye mpango huo ambao tuliaminishwa kuwa ungeweza kuleta maisha bora kwa kila mtanzania.

**Mheshimiwa Spika**, kama Serikali yenyewe inapanga na kuwasilisha hapa Bungeni, na hata baada ya kupanga inashindwa kusimamia na kutekeleza mpango wake yenyewe; ni ishara kuwa Serikali hiyo imechoka. Kambi ya Upinzani Bungeni imejiandaa vilivyo kuhakikisha kuwa Tanzania inaweka vipaumbele ambavyo vinatekelezeka na vitaweza kutatua matatizo ya watanzania kupitia Serikali itakayoundwa na UKAWA ifikapo Oktoba 2015.

**HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** nimalizie kwa kuyakumbuka maneno ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere aliyewahi kusema;

> *"Na hakutakuwa na watu wa kizazi hiki na karne hii ambao watatakiwa kujitoa muhanga kwa ajili ya maisha bora*

*katika siku zijazo wakakubali, wakati wanawaona watu wachache wakiendelea kuneemeka machoni pao bila kujali wakati ujao, wakati wao (wananchi) na watoto wao wakiendelea kuishi katika maisha duni na dhalili."*[1]

Hizi ni salamu kwa CCM ambao wanaendelea kusema kuwa 'kelele za mpangaji hazimnyimi mwenye nyumba usingizi'. Chagua UKAWA kwa mustakabali wa Taifa kwa kuwa, mwenye nyumba amejenga nyumba kwenye kiwanja cha mkopo, marejesho Oktoba 2015!

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

Esther N. Matiko (MB),

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI OFISI YA RAIS – MAHUSIANO NA URATIBU**

18.05.2015

[1] 'Reflections On Leadership in Africa' VUB University Press, 2000.